

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE
SHULE YA SEKONDARI NDEMBELA ONE.

SIMU: +255763828908 AU
+255 718416462
+255755227083

S.L.P 148
TUKUYU.

05/12/2020

KUMB. NA. NDOSS/S.5313/JOINS/VOL.1/002

JINA LA MWANAFUNZI:.....

S.L.P:.....

.....

.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA SEKONDARI KIDATO CHA
KWANZA MWAKA 2021 KATIKA SHULE YA SEKONDARI NDEMBELA
ONE WILAYA YA RUNGWE MKOA WA MBEYA.**

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii ya Sekondari Ndembela One kwa mwaka 2021. Shule ya Sekondari Ndembela One ipo umbali wa km 04 Kaskazini Magharibi mwa mji wa Tukuyu.

Masomo ya muhula wa kwanza yanaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 11/01/2021. Mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe 25/01/2021. Endapo utachelewa kuripoti Shuleni ndani ya siku 14 unaweza kupoteza nafasi yako.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 Sare za Shule.

- a) Kwa wavulana sare ya shule hii ni suruali mbili (2) rangi ya dark blue na damu ya mzee, vipande vimeambatanishwa pembeni mwa barua hii, mashati rangi nyeupe mawili mikono mifupi aina ya tetron na viatu vyeusi vya kamba kisigino kifupi na soksi nyeusi
- b) Kwa wasichana sare ya shule hii ni sketi mbili (2) rangi ya dark blue na damu ya mzee, vipande vimeambatanishwa pembeni mwa barua hii, mashati rangi nyeupe mawili mikono mifupi aina ya tetron na viatu vyeusi vya kamba kisigino kidupi na soksi nyeupe
- c) Kwa wasichana wa dini ya kiislam rangi ya hijabu iwe rangi nyeupe.
- d) Sare ya michezo kwa shule hii ni track suit ya nyeusi (adidasi).
- e) Sweta rangi ya kijani iliyokolea na tisheti ya Dark Blue yenye kola.
- f) Raba za michezo jozi moja.
- g) Tai Dark Bluu na damu ya mzee

2.2. KUTOKANA NA WARAKA WA ELIMU NAMBA 6 WA MWAKA 2015 KUHUSU UTEKELEZAJI WA ELIMU MSINGI BILA MALIPO MZAZI/MLEZI ATAKUWA NA MAJUKUMU YAFUATAYO.

- (i) Kununua sare za shule na michezo, vifaa vya kujifunzia vikiwemo madaftari na kalamu, na chakula kwa wanafunzi wa kutwa.
- (ii) Kugharamia matibabu kwa watoto wao.
- (iii) Kulipia nauli ya kwenda Shule na kurudi kwa wanafunzi wa kutwa na wanafunzi wa bweni wakati wa likizo.
- (iv) Kununua magodoro, shuka vifaa vya usafi binafsi kwa wanafunzi wanaosoma Shule za bweni na wanaoishi katika Hosteli zinazotumiwa na serikali, na
- (v) Kukemea na kutoa taarifa kuhusu mienendo inayokwenda kinyume na elimumsingi bila malipo.
- (vi) Kufuatilia mahudhurio na maendeleo ya taaluma ya watoto wao.

2.3. Vifaa vya kujifunzia darasani.

- a) Daftari (counter Books Quire 3) kumi na moja (11) kwa ajili ya Notes darasani.
- b) Daftari kumi na moja (11) ndogo (karatasi 48) kwa ajili ya mazoezi na majaribio mabalimbali.

2.4. Vifaa vya kujifunzia masomo ya sayansi na yanayohusiana na somo la hisabati;

- a) Mkebe (Mathematical set) na mathematical table (four figure).
- b) Kalamu za wino wa bluu au mweusi za kutosha.
- c) Kalamu za risasi za kutosha.
- d) Rula ya futi moja.

2.5. Mahitaji mengine ya kibinadamu ni kama ifuatavyo:-

- a) Mfagio mmoja mrefu (maarufu kama “chelewa”) na kizoleo cha takataka
- b) Jembe lenye mpini na panga/fyekeo (kwanja).
- c) Ndoo kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama vile usafi n.k.
- d) Faili moja lenye kibanio cha chuma mfano wa file hilo ni kama lililoandikwa **folder file, ultra flat file** mengine madogo kama hayo kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za wanafunzi.

3.0.SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebisha kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995 aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, wizara yenye dhamana ya Elimu nchini, chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na kisha utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni;

3.1. Muda wote uwapo mwanafunzi unatakiwa kuzingatia sana mambo yafuatayo:-

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla ni lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
- c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

- d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
- e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule ni wajibu wako wa kila siku.
- f) Kuvaa sare sahihi ya shule wakati wote unapotakiwa.
- g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- h) Kutunza mali za umma.

3.2. MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- e) Kupigana au kupiga.
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g) Kudharau bendera ya taifa
- h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba/Kusababisha ujauzito.
- i) Kuoja au kuolewa
- j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- k) Kukataa adhabu halali kwa makusudi.
- l) Kuwa na simu ya mkononi.

4.0. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYO PASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.

- a) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Form hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
- b) Form ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri na kufuata sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayo tolewa na shule.

N.B. Nyaraka tatu zilizotajwa kwenye maelezo Na. 4.0 a), b) na c) hapo juu zinatakiwa kuletwa zikiwa kwenye faili lililoagizwa kwenye kielelezo Na. 2.4 (d)

5.0 Tafadhari soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu kwa wakati uliopangwa.

Nakukaribisha shule ya Sekondari Ndembela One na kutakia maandalizi mema.

Wako,

.....

LAIBEN P. KINYUNYU

MKUU WA SHULE.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A:

To the medical officer, From:

.....

.....

.....

Re: _____

Please examine the above as to his /her physical and mental fitness for a full time Secondary school studies that may also include military training the examination should include the following categories (I, iv) each category or sub – category of which will render the application ineligible in case of a defect pregnancy (category IV) will also render a girl candidate ineligible for the cause.

- I. (a) eye sight
- (b) Hearing
- (c) Speech
- (d) Limbs
- (e) General diseases
- (f) Leprosy
- (g) Epilepsy

Other serious disease

Pregnancy

PART B: MEDICAL OFFICER

(To be completed by a government medical officer)

I have Examined the above named and consider that he/ she is physically fit for a full time secondary School studies

- (a) Eye sight
- (b) Hearing
- (c) Speech
- (d) General diseases
- (e) Leprosy
- (f) Epilepsy

- II. Neuroses
- III. Other serious diseases
- IV. Pregnancy

DATE: **SIGNATURE:**

STATION: **DATE**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
(OR -TAMISEMI)**

**HALMASHURI YA WILAYA YA RUNGWE
SHULE YA SEKONDARI NDEMBELA ONE
FOMU YA TAARIFA BINAFSI**

SEHEMU: A

1. Jina la mwanafunzi
2. Mwaka wa kuzaliwa mwanafunzi kabila la mwanafunzi.....
3. Anuani ya Mzazi/Mlezi au namba ya simu.....
4. Uhusiano Kazi yake
5. Mahali anapoishi Mwanafunzi
6. Umbali kuja shuleni ni km

Majina ya ndugu / mlezi wa karibu.

JINA LA MZAZI/ MLEZI WA KARIBU	UHUSIANO	NAMBA YA SIMU

7. **MENGINEYO KAMA YAPO**(ama Mgonjwa, yatima, mlemavu).

SEHEMU B: TAMKO LA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NDEMBELA ONE.

Mimi (Jina la Mwanafunzi)
Nimezisoma na kuzielewa sheria, kanuni na taratibu za shule na kwamba niko tayari/ siko tayari kuzifuata.

Sahihi ya mwanafunzi Tarehe

SEHEMU C: TAMKO / AHADI YA MZAZI /MLEZI

Mimi (jina la mzazi/ mlezi) ambaye ni mzazi wa mwanafunzi ninaahidi kwamba nitatekeleza/ sitatekeleza maagizo na mahitaji yote muhimu ya shule kama nilivyoelekezwa na kwamba niko tayari/ siko tayari kushirikiana na uongozi wa shule katika suala zima la malezi na maadili mema ya mtoto wangu ili kuinua Taaluma na nidhamu yake.

Sahihi ya Mzazi / Mlezi tarehe